TANGAZO LA SERIKALI NA. 407 la tarehe 24/5/2025

SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI,

(SURA YA 44)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 64)*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA TARATIBU ZA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO YA UKIUKWAJI WA MISINGI YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI ZA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 350 la 2023

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Taratibu za Kushughulikia Malalamiko ya Ukiukwaji wa Misingi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi za mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Taratibu za Kushughulikia Malalamiko ya Ukiukwaji wa Misingi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi za mwaka 2023 ambazo katika marekebisho haya zitarejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 4

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 4 kwa -

(a) kufuta na kuandika upya kanuni ndogo ya (1) kama ifuatavyo:

"(1) Mtu au kikundi cha watu kitakachobaini ukiukwaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi au kutoridhishwa na uamuzi wa mkusanyaji au mchakataji kuhusiana na taarifa binafsi kitaweza, ndani ya muda wa siku ishirini na moja baada ya kubaini ukiukwaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi au uamuzi wa mkusanyaji au mchakataji, kuwasilisha kwa Tume malalamiko kwa kutumia fomu Na. 1 iliyoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi.";

(b) kufuta maneno ya utangulizi ya kanuni ndogo ya (3) na kuyaandika upya kama ifuatavyo:

"(3) Endapo malalamiko yaliyowasilishwa

chini ya kanuni ndogo ya (1) ni ya kikundi cha watu, malalamiko hayo yataambatishwa na-"; na

(c) kuweka maneno "Ndani ya siku tano" kabla ya neno "Baada" lililopo mwanzoni mwa kanuni ndogo ya (5).

Marekebisho ya kanuni ya 8

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 8 kwa kufuta maneno "muda uliotolewa" na badala yake kuweka maneno "muda wa siku saba".

Marekebisho ya kanuni ya 12

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 12(3) kwa kuongeza maneno "ambao kwa vyovyote hautazidi siku saba" mara baada ya neno "Tume".

Marekebisho ya kanuni ya 13

5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 13(1) kwa kufuta na kuandika upya kanuni ndogo ya (1) kama ifuatavyo:

"(1) Tume itapaswa, baada ya kupokea utetezi kutoka kwa mlalamikiwa au majibu ya utetezi kutoka kwa mlalamikaji, kama yapo, kuchunguza suala husika na kujiridhisha endapo-

(a) mlalamikaji ana maslahi katika suala ambalo lalamiko linahusika; au

(b) lalamiko siyo la uzushi au halina msingi.".

Dodoma,
18 Aprili, 2024

NAPE M. NNAUYE
*Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari*